**MACHAKOS UNIVERSITY**
**SCHOOL OF HUMANITIES AND SOCIAL SCIENCES**
**DEPARTMENT OF LINGUISTICS AND LANGUAGES**

# AKS 100: INTRODUCTION TO THE STUDY OF LANGUAGE

**MAAGIZO**: Jibu swali la **kwanza** na mengine **mawili**.

1. (a) Tambua mambo sita yanayoweza kutofautisha utendaji wa lugha na umilisi wa lugha.

(alama 6)

(b) Tofautisha jozi zifuatazo za istihali kama zinavyotumiwa katika taaluma ya isimu.

(i) 'Langue' na 'parole' (alama 4)

(ii) Lugha na isimu (alama 4)

(iii) Diakronia na sinkronia (alama 4)

(a) Dhihirisha kuwa isimu ni sayansi. (alama 12)

1. (a) Jadili viwango vyovyote vitano vya isimu. (alama 10)

(b) Tambua kiungo cha kimsingi kwa kila kiwango cha kiisimu ulichojadili. (alama 10)

2. Eleza uhusiano wa isimu na taaluma zifuatazo.

(a) Sosholojia (alama 4)

(b) Historia (alama 4)

(c) Falsafa (alama 4)

(d) Anthropolojia (alama 4)

(e) Fasihi (alama 4)

3. Kwa kurejelea nadharia ya kisayansi fafanua chanzo cha lugha. (alama 20)

4. Toa maelezo kuhusu mikabala ifuatayo ya isimu.

   (a) Mkabala wa daikronia. (alama 10)

   (b) Mkabala wa sinkronia. (alama 10)

5. (a) Fafanua aina zifuatazo za lugha. (alama 10)
   (i) Krioli
   (ii) Pijini
   (iii) Lingua franka
   (iv) Lugha rasmi
   (v) Lugha ya taifa
   (c) Jadili umuhimu wa kozi hii kwa mwanafunzi wa Kiswahili. (alama 10)

**MACHAKOS UNIVERSITY**
**SCHOOL OF HUMANITIES AND SOCIAL SCIENCES**
**DEPARTMENT OF LINGUISTICS AND LANGUAGES**
**AKS 101: LANGUAGE SKILLS IN KISWAHILI**

**MAAGIZO**: Jibu swali la **kwanza** na mengine **mawili**.

1. (a) Eleza namna **vikwazo vya ujumbe** na **vikwazo vya mpokezi** vinavyoathiri mawasiliano.

(alama 10) (b) Pendekeza mbinu za

kuepusha vikwazo hivi katika mchakato wa mawasiliano.

(alama 10)

(c) Fafanua vipengele mbalimbali vya mawasiliano. (alama 10)

2. (a) 'Mawasiliano huwa ya viwango vingi.' Jadili. (alama 10)

(b) Dhihirisha mambo ya kimsingi katika uandishi wa kumbukumbu za mihadhara.

(alama 10)

3. (a) Jadili mambo ya kuzingatia katika maandalizi ya hotuba. (alama 10)

(b) Onyesha jinsi ya kupunguza makosa ya tahajia katika maandishi yako. (alama 10)

4. (a) Tambua sababu za kutokuwa na usikilizaji bora. (alama 10)

(b) Eleza njia ainati za kutatua changamoto za usikilizaji bora. (alama 10)

5.Thibitisha kuwa alama zifuatazo za uakifishaji huwa na matumizi tofautitofauti.

(a) Herufi kubwa (alama 4)

(b) Kitone (alama 4)

(c) Mstari (alama 4)

(d) Koloni (alama 4)

(e) Kinyota (alama 4)

**AKS 200: PHONETICS AND PHONOLOGY**

Jibu swali la kwanza na mengine mawili.

1a) Eleza dhana hizi; fonetiki na fonolojia. (Alama 10)

b) Chagua irabu mbili na konsonanti tatu uzieleza zifa za kiaustika kwa kila sauti. (Alama 20)

2. Fafanua dhana ya uyeyushaji katika Kiswahili kwa kutoa mifano mitano. (Alama 20)

3. Andika maneno haya ukitumia AKIKI.
a) mvua b) nyanya c) ghadhabu d) ungio e) sharashamra f) yaya g) changarawe (Alama 20)

4. Eleza dhana hizi:
a) kiimbo b) shadda c) kiimbo d) utonimu (Alama 20)

5. a) Silabi ni nini? (Alama 5)

b) Fafanua maumbo yoyote matano ya silabi za Kiswahili. (Alama 15)

## Second Year, Examination for Bachelor of Education Arts/BA

### AKS 201: INTRODUCTION TO KISWAHILI LITERATURE

**Tarehe:** **Muda:**

---

***Maagizo: Jibu <u>Swali la Kwanza</u> na Mengine Mawili.***

1. (a) Eleza aina tatu za sanaa kwa mujibu wa Muhando wa Balisidya (1976) (Alama 8)

(b) Fafanua kwa kifupi mitazamo miwili inayoeleza asili ya sanaa (Alama 6)

(c) Eleza dhana zifuatazo: (Alama 10)

(i) Majazi

(ii) Kinaya

(iii) Dhamira

(iv) Maudhui

(v) Tarihi

(d) Fafanua aina tatu za nyimbo. (Alama 6)

2. (a) 'Fasihi simulizi ya Kiswahili inakabiliwa na tisho la kufa.' Eleza sababu zinazochangia kufa kwa fasihi simulizi. (Alama 10)

(b) Pendekeza mikakati ya kuiokoa fasihi simulizi isife. (Alama 10)

3. Jadili uhusiano baina ya fasihi simulizi na fasihi andishi. (Alama 20)

4. Eleza sifa zinazotofautisha utanzu wa riwaya na hadithi fupi. (Alama 20)

5. Kwa kutoa mifano, jadili aina tano za tamthilia ya Kiswahili. (Alama 20)

**AKS 300: MORPHOLOGY AND SYNTAX**

Jibu swali la kwanza na mengine mawili.

1 a) Kishazi ni nini? (Alama 10)

b) Chambua miundo ya sentensi hizi ukitumia vionyesho (SPCA) kwa mujibu wa Halliday:

i) Mtoto amepelekwa hospitali haraka.
ii) Alikimbia kumpokea mgeni.
iii) Mama ni mgonjwa.
iv) Kariuki aliendesha baskili kwa uangalifu.
v) Kwa haraka alienda dukani. (Alama 20)

2. a) Eleza dhana ya ngeli. (Alama 5)

b) Ainisha ngeli za Kiswahili kisintaksia na uonyeshe udhaifu wake. (Alama 15)

3. Jadili umuhimu wa viambishi katika usahihi wa sentensi ya Kiswahili. (alama 20)

4. Jadili aina mbalimbali za vishazi tegemezi katika Kiswahili. (Alama 20)

5. Fafanua unyambuaji katika Kiswahili na vikwazo vyake. (Alama 20)

# MACHAKOS UNIVERSITY
# SCHOOL OF HIMANITIES AND SOCIAL SCIENCES
# DEPARTMENT OF LINGUISTICS AND LANGUAGES
## Second Year First Semester Examination for Bachelor of Education/ Bachelor of Art
## AKS 301: KISWAHILI STRUCTURE

**Maagizo**: Jibu swali la **kwanza** na mengine **mawili**. Time: 2 Hours

1. (a) Fafanua dhana hizi: (alama 6)
   - (i) Fonimu
   - (ii) Foni
   - (iii) Alofoni

   (b) Ainisha kononanti za Kiswahili kwa kuzingatia kigezo cha mahali pa kutamkia. (alama 14)

   (c) Eleza kanuni mbalimbali zinazotawala mfuatano wa irabu za Kiswahili katika maneno. (alama 10)

2. (a) Dhihirisha mikondo yoyote mitano ya kifonolojia katika lugha ya Kiswahili. (alama 10)

   (b) Nyambua vitenzi vya kiswahili katika kauli tano tofauti. (alama 10)

3. (a) Tambua na ueleze aina sita za nomino. (alama 12)

   (b) Fafanua aina kuu za vielezi vya Kiswahili. (alama 8)

4. Mbaabu (1992) anapendekeza uainishaji wa ngeli za Kiswahili kwa kuzingatia vionyeshi vya karibu.

   (a) Jadili makundi ya ngeli aliyobainisha. (alama 12)

   (b) Thibitisha kuwa uainishaji huu ni bora kuliko unainishaji wa awali. (alama 8)

5. (a) Tofautisha kai ya:

   (i) Kiima na kiarifu (alama 4)

   (ii Shamirisho na chagizo (alama 4)

   (iii) Kirai na kishazi (alama 4)

(b) Kwa kuzingatia kigezo cha muundo tunaweza kuainisha sentensi tofauti. Eleza.

(alama 8)

Aks 302 THEORIES OF LITERATURE AND LITERARY CRITICISM

**Tarehe:** **Muda: 2hrs**

---

***MAAGIZO:*** **Jibu la <u>Kwanza</u> na mengine <u>Mawili</u>**

1. (a) Fafanua dhana zifuatazo:

(i) Nadharia ya uhakiki (alama 2)

(ii) Kutolea uamuzi kazi ya kifasihi (alama 2)

(b) Eleza sifa za fasihi ya Kiswahili katika misingi ya kirasimi (alama 6)

(c) Eleza shabaha tano za uhakiki wa fasihi (alama 10)

(d) Tambua sifa tano za Uhalisia wa Kijamaa (alama 10)

2. Kwa kutoa mifano, jadili aina mbalimbali za uhakiki (Alama 20)

3. (a) Fafanua sifa za fasihi kwa mujibu wa wataalamu wafuatao wa urasimi mkongwe:

(i) Plato (Alama 6)

(ii) Aristotle (Alama 6)

(b) Eleza sifa nne za tamthilia ya tanzia (Alama 8)

4. Jadili jinsi nadharia ya Ufeministi inavyoweza kutumiwa kuielewa riwaya ya **Siku Njema** (Ken Walibora 1996). (Alama 20)

5. (a) Kwa kutoa mifano, fafanua mbinu tatu za kuzalisha nadharia (Alama 6)

(b) Eleza sura tano za nadharia (Alama 10)

(c) Taja mawazo matatu ya mwanafalsafa wa Kirumi (Horace) kuhusu fasihi kwa jumla (Alama 4)

## University Examination for 2021/2022

## Third Year, Second Semester Examination for Bachelor of Education (Arts)/BA

**AKS 303 CONTEMPORARY KISWAHILI NOVEL AND PLAY**

| **Tarehe** | **Muda** |
|---|---|

***Maagizo: Jibu swali la kwanza na mengine mawili.***

1. (a) Eleza sifa tano za kimuundo wa tamthilia ya kisasa. Alama 10)

(b) Fafanua sifa tano za mhusika wa riwaya kisa (Alama 10)

(c) Kwa kutoa mfano, fafanua istilahi zifuatazo: (Alama10)

(i) Tanakali za sauti

(ii) Nidaa

(iii) Kuchanganya ndimi

(iv) Kuhamisha ndimi

(v) Tasfida

2. Fafanua sifa bainifu **kumi** za tamthilia ya Kiswahili. (Alama 20)

3. Jadili mbinu za sanaa zilizotumiwa na Said Ahmed Mohamed katika tamthilia ya ***Amezidi*** (Mohamed 995) (Alama 20)

4. Kwa kutoa mifano, eleza mikitadha mitatu iliyochangia ukuaji wa riwaya ya Kiswahili (Alama 20)

5. Kwa kutoa mifano, ainisha riwaya za Kiswahili kimaudhui na kimtindo (Alama 20)

**AKS 304: TRANSLATED KISWAHILI NOVEL AND PLAY**

Jibu swali la kwanza na mengine mawili.

1. a) Fafanua dhana ya fasihi tafsiri. (Alama 10)

   b) Eleza mchango wa fasihi tafsiri katika kuendeleza fasihi ya Kiswahili. (Alama 20)

2. Jadili mbinu tano za kisanii katika riwaya ya *Shamba la Wanyama* (George Orwell) (Alama 20)

3. Fafanua mafunzo yoyote manne yanayopatikana katika tamthiliya ya *Masaibu ya Ndugu Jero*. (Alama 20)

4. Chagua riwaya tafsiri yoyote uliyoisoma na ujadili matumizi ya lugha. (Alama 20)

5. "Kudra ya Mungu, binadamu hawezi kujikwamua". Thibitisha kauli hii ukirejelea tamthiliya ya *Mfalme Edipode* (Sophocles). (Alama 20)

**AKS 402: KISWAHILI POETRY**

Jibu swali la kwanza na mengine mawili.

1. a) Arudhi katika ushairi ni nini? (Alama 5)

   b) Jadili mgogoro wa arudhi katika ushairi. (Alama 25)

2. Jadili chimbuko la ushairi ukizingatia a) mtazamo wa kidhanifu b) mtazamo wa kiyakinifu

   (Alama 20)

3. Fafanua istilahi hizi za ushairi kwa kutoa mifano mwafaka:

   a) Ubeti b) Kina c) Mizani d) Kibwagizo e) Muwala (Alama 20)

4. Eleza tanzu hizi za ushairi na tofauti zilizopo:

   a) Utenzi/Utendi

   b) Shairi

   c) Wimbo (Alama 20)

5. a) Taswira ni nini? (Alama 5)

   b) Eleza matumizi ya taswira katika ushairi wa Kiswahili. Toa mifano mwafaka. (Alama 15)

## University Examination for 2021/2022

## Fourth Year, Second Semester Examination for Bachelor of Education (Arts)

**AKS 403 FASIHI SIMULIZI**

**Tarehe** **MUDA:**

---

***Maagizo: Jibu swali la kwanza na mengine mawili.***

1. (a) Fafanua dhana zifuatazo: (Alama 6)
   (i) Nyiso
   (ii) Ngomezi
   (iii) Kitendawili
   (b) Eleza sifa nne za methali (Alama 4)
   (c) Kwa kutumia vigezo tofauti, ainisha fasihi simulizi katika makundi matano. (Alama 10)
   (d) Fafanua umuhimu wa ngomezi katika jamii (Alama 10)

2. Fafanua matatizo matano yanayotishia kesho ya fasihi simulizi na upendekeze njia za kukabiliana nayo. (Alama 20)

3. (a) Kwa kutoa mifano, fafanua aina tano za ngano za fasihi simulizi. (Alama 10)

   (b) Eleza sifa tano za miviga (Alama 10)

4. (a) Kwa kujikita kwenye kigezo cha tamathali za usemi, eleza miundo mitano ya vitendawili. (Alama 10)

   (b) Eleza sifa tano za vitendawili. (Alama 10)

5. Eleza uhusiano baina ya fasihi simulizi na fasihi andishi (Alama 20)

**AKS 413: COMPERATIVE LITERATURE**

Jibu swali la kwanza na mengine mawili.

1. a) Fasihi linganishi ni nini? (Alama 10)

   b) Chagua vipengele vinne vya fasihi na ueleze jinsi hulinganishwa katika kazi mbili za fasihi. (Alama 20)

2. Linganisha wahusika wakuu kitabia katika riwaya za *Rosa Misitika* (Kezilahabi) na *Maisha Kitendawili* (Habwe). (Alama 20)

3. Eleza tofauti tano kati ya hadithi fupi za kale na za kisasa. (Alama 20)

4. Kwa kurejelea tamthilia mbili ulizozisoma, linganisha mbinu za kisanii. (Alama 20)

5. Linganisha ujumbe katika jozi hizi za methali:

   a) Haraka haraka haina baraka/Chelewa chelewa utamkuta mtoto si wako.

   b) Mkataa la mkuu huvunjika guu/Sikio halipiti kichwa.

   c) Uzuri wa mkakasi ndani kipande cha mti/Uzuri wa nyumba si mlango

   d) Mwana msikivu haambiwa sana/Papo kwa papo kamba hukata jiwe. (Alama 20)